

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**

**MKOA WA KILIMANJARO**

Simu : 027-2758441  
Fax : 027- 2756102



**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.**

S. L.P. 27  
**HAI**

Tarehe 19/08/2019.

## **TANGAZO LA ZABUNI**

Halmashauri ya Wilaya ya Hai inatangaza zabuni ya kukodisha magari kwa ajili ya kazi maalumu itakayofanyika tarehe 11/09/209 na 12/09/2019 ndani ya mipaka ya Halmashauri. Magari yanayohitajika yanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

1. Liwe na uwezo wa kubeba abiria 8, 20, 25, 35 au 40.
2. Liwe na dereva mwenye leseni yenyé hadhi ya kuendesha magari ya abiria
3. Liwe na Bima hai (Valid Insurance Cover)
4. Kwa gari lenye uwezo wa Kubeba abiria 8 ni lazima liwe na 4WD

### **ZABUNI HII INATANGAZWA CHINI YA MASHARTI YAFUATAYO:-**

1. Kwa mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuhakikisha gari linafika yadi ya Halmashauri saa 2.30 asubuhi ya tarehe **10/09/2019**.
2. Mwombaji atakayeshinda zabuni awe tayari kupeleka gari lake sehemu yoyote atakayopangiwa ndani ya Wilaya ya Hai.
3. Mwombaji ainishe kwenye maombi yake akionyesha aina ya gari, namba ya usajili, bei ya kukodi gari kwa siku moja, uwezo wa gari (idadi ya abiria) na namba ya simu yake kwa ajili ya mawasiliano.
4. Maombi ya zabuni yafungwe kwenye bahasha na kuandikwa juu pembedi **zabuni ya kukodi gari** na yatumwe kwa **Katibu wa Bodi ya Zabuni(W)**, S.L.P 27 Hai na zipelekwe **ofisi ya ugavi na manunuvi**.
5. Mwombaji wa Zabuni atalazimika kumlipa Dereva wake posho ya kujikimu
6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **23/8/2019 saa 8.00 mchana**.
7. Halmashauri ya Wilaya ya Hai hailazimiki kukubali kima cha zabuni cha juu au cha chini.
8. Kazi inayokusudiwa kufanywa na magari haya ni **NYETI** hivyo ni lazima mwombaji ajiridhishe kuwa gari lake liko katika hali nzuri ya kumudu kazi hiyo bila kuharibika.
9. Gari liwe na ubora na safi.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Sintoo'.

**Yohana E. Sintoo**

**MKURUGENZI MTENDAJI.**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI.**

*MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HAI*